TUSISITE KUABUDU KWA KUMALIZIKA MWEZI WA RAMADHANI

BAADA YA Waislamu kumaliza kufunga mwezi mzima Mtukufu wa Ramadhan, hatuna budi kuwapa hongera; kuwahani na kama ilivyo desturi kuwapa mkono wa IDD. Kwa wale waliokuwa wakiunga, ni budi kuwapongeza kwa kuweza kwao kujinyuma chakula, vinywaji na starehe nyingine, na pia wakaweza kuzishinda nyoyo zao na macho yao katika nyanja za matamanio. Hawa ni katika Minaffaaizin.

Na kwa wale ambao walishindwa kutekeleza wajibu huu, huo twawambia ole wao. Hata hivyo twawauliza uroho wao umefika wapi? Wengine twaelewa kwamba wliacha kufunga kwa sababu za kiaffya ya mwili, lakini wengine walikuwa wakijitafutia magonjwa ua urongo bure. Hawa twawambia kwamba janja yao, Mungu aielewa vyema.

Ramadhano ya mwaka huu, kama watu wasemavyo, haikukosa barka zake. Kwanza twamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kueneza neema zake na riziki zake hata ikawa nchi yote ikawa imeenewa na chakula. Pili twaipongeza Serikali yetu ya Nyayo kwa kufanya taratibu zote hadi usambazaji wa chakula ukawa wa kutosheleza. Waislamu wameona kwamba katika mwezi mzima wa Ramadhani walipata unga, mchele ma mahitajio mengine bila ya dhiki yoyote.

Waislamu wakimaliza ibada yao ya kufunga, pia wana wajibu mkubwa wa kutoa shukurani nyingi kwa wana zuoni na mashekhe ambao walijitolea wakati wao wa mapumziko na kuwatolea waadhi na kuwafasiria Quran Tukufu pamoja na nyendo za Mtume Muhammed (SAW). Hiyo ilikuwa ni nja nzuri ya kupitishia masaa ya saumu.

Sasa twataka kuwahoji Waislamu ambao kwao wao, dini hufanywa mwezi wa Ramadhani pekee, kwa nini iwe hivyo? Jee kuna Mungu wa Ramadhani mbali na Mungu wa mala mchana mbali? Ikiwa wana amini na wanaitakidi kuwa Mungu wa Kuabudiwa kwa haki ni mmoja, basi kwa nini siku nyengine astahiki kuabudiwa na siku nyengine zistahiki kuabudiwa? Sivyo hivo.

Kuna Waislamu ambao waliweza kusali vipindi vyote vitano vya sala katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, lakini Waislamu hawa hawa mara tu baada ya kusali sala ya Idd, msikiti utawatamani, na itabidi misikiti istahamili kwa muda wa myezi kumi na moja ndipo ione tena sura za watu hawa. Jee ndugu zetu hivi ndivyo? Hebu fikiria wewe Idi Mwenyezi Mungu angekuzuilia riziki kwa muda wa myezi yote kumi na moja na akakuruzuku mwezi wa Ramadhani peke yake, jee huyo wengemuona ni Mungu wa sampuli gani?

Ikiwa ulijinyima miraa kwa muda wa mwezi mmoja na ikawa hukufa kwa njaa, basi kwa nini uirudie tena? Au unataka kuwapa fikra Wameru kwamba Waislamu ni wachamungu mwezi mmoja pekee katika kalenda na myezi yote iliyobaki na maasi wakubwa sana? Ikiwa ulijizuilia na ulevi mwezi mzima na ikawa hukufa kwa kiu, kwa nini unudi tena Fantanela? Jee unataka ukenda huko walevi wenzako wakakupokee kwa nderemo, na waseme fulani alikua akimwogopa Mungu katika mwezi wa Ramadhani lakini sasa hamchi tena. Huoni kuwa huko ni kupakwa matope Waislamu na dini yao? Hatukwambii kuwa uwewanazuoni lakini kipindi tu kisikupite. Maana vile kusali mara tano kila siku, ndiko kutakako kupunguzia maasia yako na mwisho ukaona umepunguza maasia na hatimaye kuyawacha kabisa.

Basi nakwambia wewe fulani, na wewe na wewe pia fulani usikate guu lako tena msikitini, usighilibiwe na ujana. Kumbuka kuwa ujana ni kama moshi ukienda haurudi tena. Basi naiwe hivyo Awam baada awam, Sinin baada Sinin.

Sasa tusherehekee Idd-el-Fitri kikamilifu

na FARAJ DUMILA

WALI WAISLAMU waliotekeleza zile ibada za kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani huwa wakijihisi kufaulu kukubwa kwa kumpika na siku huu ya "Idd-el-Fitr". Kule kusherehekea huku kwa siku kuu hii ni kielezo cha kufaulu kwao katika kujizuia na maovu na kujingiza katika hali ya kuu ya uwanadamu.

"Idd-el-Fitr" ni siku kuu yenye furaha isyoelezeka kwani Waislamu hujona amejifunza mengi. Kule kuweza kujinyima si kufanya maovu ndio kunakomtia katika hali ya kujifikiria wanaoishi sasa ana moyo thabiti wa kuweza kujiepusha na maovu na kujikumbusha zaidi na mambo mengi ambayo mafunzo ya dini yake ya kukoteza.

Ndipo katika kusherehekea siku kuu hii tukawaona Waislamu wanajamba na kuwapamba watoto wao na wake zao kwenda kwa kila lile pambo wanaloweza kuwapatia. Sifa ya dunia hudhihiri wazi kwani kila Mwislamu hupendelea kumpa mwenzwe kile kidogo alicho nacho ili wawe wamebadilishiana zawadi. Hidaya kubwa wanaopeana kila mara ni kule kusema "Idd Mubarak" — ikiwa na maana kwamba kila mambo mema na ya heri yawe yakikufikia kila mara na nendelee na hali hii ya furaha kila siku.

Katika huu mwezi mtukufu wa Ramadhani Waislamu walitekeleza wajibu wao hupata kujua kwamba kule kufanya sema ndio sifa ya mtu mwenye utu.

Lakini jingine analolitia maanani sana ni upendo wa nchi yake kama vile alivyouswa katika hadithi ya Mtume Mohammed (S.A.W.) anyosema: "Kupenda nchi yako ni miongoni mwa imani". Vile akijihisi kwamba wananchi wote, wa dini tofauti ni wa kama ndugu zake anaofaa kushirikiana katika ujenzi wa nchi ndio huko kuthibitika imani yake katika dini yake na hasa kwamba Mwezi Mtukufu umemkumbusha funzo hili muhimu la kupendana na wananchi wenzake kwa manufaa ya maendeleo ya nchi.

Siku huu ya "Idd el Fitr" inampatia Mwislamu mwema mafunzo chungu nzima miongoni mwao ni huko ambako mitakwa awe akiendelea kujifunza hadi siku ya kwenda kwake Allahu.

Idd Mubarak!

FARSY ANAIOMBEA UFANISI SERIKALI NA NCHI YA KENYA

SHEIKH A. S. EL-FARSY

KWA niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba ya Waislamu wote wa nchi hii yetu tukufu ya Kenya, nachukua fursa hii, katika kuadhimisha mwisho wa mwezi mtukufu wa Ramadhani, ilhali ya kusherehekea Idd-ul-Fitri, kuiombea Serikali yetu tukufu inayoongozwa na mpendwa baba wa Taifa Muheshimiwa Bwana Daniel Arap Moi.

Naiombea ufanisi Serikali yake ya Nyayo, chama chake cha Kanu, baraza lake la Mawaziri pamoja na bunge lote pia. Mwenyezi Mungu amtuwilishe umuri Rais yeye na aila yake na azidi kuiongoza nchi yetu hii ya Kenya kwa salama na amani.

Mungu ailinde nchi yetu na maadui zake, atuondoshee balaa na maradhi na pia atuzidishie neema za chakula pamoja na maji safi.

Mwenyezi Mungu uwabariki Waislamu na raia wote waishi kwa umoja na kupendana bila ya udhia na fitina. Mola awalinde watoto wote wa Nyayo awanusuru na ufisadi na awaongozee ili na wao waje walifae na walilinde Taifa lao siku zijazo.

Na nikimaliza, kwa mintaraf ya Waislamu wa Mombasa, nawapelekea mkono wa Idd kwa ndugu zao wa Kiislamu kote nchini.

Abdalla Saleh El-Farsy,
Kadhi Mkuu,
MOMBASA.

NYUNDO ITASHEREHEKEA IDD KWA BHALO NA HARAMBEE

MIMI Mwenyekiti wa Nyundo Football Club, nachukua fursa hii kupeleka Mkono wa Idd Mubarak kutoka kwa timu yetu na wachezaji wake kwenda kwa Timu za mchezo wa Soka nchini kote na khususan timu za hapa mjini Mombasa.

Nina furaha kwa vile mechi za mini-ligi zinavyoendelea na nazidi kuomba mashairikiano ya timu zote kwa kuendeleza soka hapa Pwani. Nikisemea kidogo kuhusu klabu yangu, napenda kueleweka kwamba tuna shida ya fedha kwa muda huu za kupelekea klabu chetu mbele, kwa hivyo nawaomba wapenzi wa kandanda wote popote pale walipo, watuletee misaada ya aina yoyote ile ili tupeleke mbele klabu chetu.

Pia nachukua fursa hii, kuwatangazia wanamichezo wote kwamba siku ya Jumatatu tarehe 3 Agosti, mnamo saa moja ya usiku hapo katika ukumbi wa Lohana, tutakuwa na tafrija karamu na muziki utakaoporomoshwa na Juma Bhalo. Kiingilio ni shillingi ishirini pekee, na pia kutakuwa na bahati nasibu.

Tafadhalini fikeni kwa wingi muje musaidie ndugu zenu. Na sisi tutafika kwa yoyote atakayeomba msaada, kwani hiyo ndiyo harambee ya Nyayo.

Mwenyekiti,
Nyundo Football Club,
MOMBASA.

IDD MUBARAK

TUNACHUKUA fursa hii kupeleka salamu zetu za Idd-ul-Fitri kwa Rais wetu Mtukufu Muheshimiwa Daniel Arap Moi, Mawaziri wetu, Manaibu Mawaziri na Wanabunge wetu wote wa hapa Kenya. Tunamuombea Rais wetu maisha marefu na afya niema ili aendelee kutuongoza kwa mapenzi, huruma, umoja na amani. Amin.

Wa aidha tunawatakia Waislamu wote Idd-ul-Fitri ya kheri, baraka, amani na furaha Mola inshaala atujaalie ni wenye kupendana, kusaidiana na tuoneshane ya kheri na kukatazana mabaya.

Kwa mintaraf ya M.W.I., twapenda kutoa shukurani zetu za dhati kwa kila aliyejitolea kutusaidia kwa nja yoyote ikiwa ni kwa mali au maoni mazuri ambayo kwayo tumeweza kukita kama hivi leo tunavyoonekana. Inshaala misaada yao haitakuwa ya mwisho bali itakuwa ya mwanzo.

Na wale ambao hawajawahi kutabaruk na sisi, inshaala Mola atawapa uwezo na moyo wa kutoa kama vile Quran ilivyosema; Limithli hadha falyatanafasi almutanafisuun.

Hatuna budi kumtolea Mwenyezi Mungu shukurani nyingi kwa kutuwezesha kukikamilisha Ramadhani yote nzima na akatupa nguvu tukasali na Sala za taraweikh, Inshaalla saumu zetu ziwe makubul na Mola atulipe thawabu nono kwa twaa yetu kwake.

Kama tulivyoona kwamba katika Mwezi wa Ramadhani, ilibidi tusimamishe baadhi ya mipango yetu na shughuli zetu, lakini mara tu baada ya kwisha funga Suna za Sita, tutaendelea na ratiba zetu kama kawaida. Twapenda kuwakumbusha tena kwamba katika Islamic Centre, kila Jumatatu na Alhamisi, tangu saa nane mchana hadi kumi jioni, na pia kila Jumamosi na Jumapili saa nne asubuhi hadi saa sita, huwa tuna darasa za watoto. Na Jumatatu na Jumanne saa kumi na nusu alasiri hadi kufikia Magharibi, huwa tuna darasa za mabibi.

Kadhalika Jumanne, Jumatano na Ijumaa, tangu jioni hadi magharibi huwa tuna mafunzo ya kupunguza mafuta na vitambi kwa mabibi pekee.

Na mwisho twapenda kutangaza kwamba siku ya Jumatatu tarehe 3 Agosti, saa tisa mchana tutakuwa na karamu ya watoto wadogo (wadogo wa myaka sio wadogo wa vimo) kiingilio ni shillingi tano tu.

Na siku ya Jumapili tarehe 9 Agosti itakuwa ni zamu ya mabibi kutanyiwa karamu (mabwana siku hiyo watapata uhuru) mnamo saa mbili usiku na kiingilio ni shillingi kumi na tano kwa wanachama. Ahsanteni.

Mwenyekiti,
Muslim Women's Institute,
MOMBASA

WALII Sheikh Abagadah ametoa mkono wa IDD kwa waislamu wote nchini baada ya mfungo wa mwezi mtuku wa Ramadhan. Anawasihi waislamu wote kuzatiti msimamo na itikadi ya dini ya kiislamu ambayo nguzo yake moja ni kuazimisha mwezi mtukufu wa Ramadhan kinadharia na kwa vitendo. Anamwoombea dua Rais Moi pamoja na Serikali yake tukufu.

COASTWEEK JISHINDIE

Miavuli maridadi katika shindano jipya la kujaza

SWAHILI CROSSWORD NO. 123



JINA .....

SANDUKU LA POSTA .....

.....

KWENDA KULIA:

1. Jina la zamani la mji wa Mombasa.
5. Mtoto wa ng'ombe.
7. Wewe
8. Kinyume cha P.M.
10. Ukavu, aradhi isiyo na maji.
12. Kidonda kikubwa.
13. United Kingdom.
14. Kitambulisho cha mtu.
15. Ua changa.
16. Safisha, toa uchafu
17. Tibu, fanyia dawa mtu.

KWENDA CHINI:

1. Chombo cha muziki
2. Ngoma kubwa.
3. Sema.
4. Weka juu ya jiko.
6. Zuia vita.
9. Teketea.
11. Panga gutu.
14. Mahali pa taka.
15. Tosha, basi.

Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 122

Walter Kingi Chengo, Sanduku la Posta 274, MALINDI.

Simeon Tawa, c/o Jimba F.P. School, P.O. Rabai, RURUMA.

Master Kavulunze D. Mulwa c/o D. M. Kimyunge, Sanduku la Posta 46550, NAIROBI.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 122 —

KWENDA KULIA:

1. TEMBO, 6. TUNZA, 7. RINDA, 8. MKATE, 10. ETI, 12. WA, 13. IANZE, 15. IMBA, 17. UBAO, 19. FURAHI.

KWENDA CHINI:

1. TARISHI, 2. MENDE, 3. OTAMIA, 4. ONJA, 5. WAMEA, 9. TWEKA, 11. TIARA, 14. NDUI, 16. MTU, 18. OA.

Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi watatu kila baada ya wiki mbili watapata miavuli maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LIMITED, Mombasa.

Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 12.8.81 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.